HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE KATIKA SHEREHE YA KUUKARIBISHA MWAKA WA 2011 KWA WENZA WA MABALOZI – IKULU TAREHE 14 JANUARI, 2011.

Habari za jioni.

Ninawashukuru sana kwa kuitikia mwaliko wangu wa kuhudhuria halfa hii ya jioni ya kusheherekea Mwaka Mpya. Ahsanteni sana kwa kuja na karibuni sana. Kama ilivyokuwa katika halfa ya mwaka jana, ningependa kutumia fursa hii kuwashukuru sana kwa ushirikiano wenu. Jioni ya leo pia tumepata fursa nyingine kubadilishana mawazo juu ya mambo yanayotugusa binafsi na mataifa yetu.

Pamoja na kuwakaribisha, natambua kuwa miongoni mwenu, mpo ambao hii ni mara yenu ya kwanza kujumuika nasi hapa. Napenda kuwakaribisheni sana Tanzania, mjisikie mko nyumbani.

Naamini kuwa kama wengine waliowatangulia, mtafurahia muda wenu mtakaoishi hapa nchini, kwani Tanzania ina watu wakarimu wenye upendo na urafiki. Vile vile inao utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii na baadhi yake ni maajabu na urithi wa dunia.

Tuna vivutio kama vile; Mbuga ya Serengeti, Hifadhi ya Ngorongoro Crater, Mlima Kilimanjaro na Visiwa vya Zanzibar, pamoja na maeneo ya kihistoria. Bila shaka mtapata fursa ya kujifunza mila na tamaduni zetu pamoja na lugha yetu ya Kiswahili ambayo inaenea kwa kasi barani Afrika na kwingineko duniani. Ni imani yangu kwamba mtafurahia mandhari ya nchi yetu na ukarimu wa wenyeji wake. Karibuni sana.

Wageni waalikwa,

Waliokuwapo mwaka jana katika sherehe kama hii watakumbuka kuwa nilieleza dhamira yangu ya kutoa mchango wangu katika kuwaendeleza watoto wa kike kielimu; kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Nilielezea nia yangu ya kushiriki katika juhudi za kuongeza na kuboresha upatikanaji huduma ya afya ya uzazi kwa akina mama, ili ziwepo sehemu nyingi zaidi na kuhamasisha wanawake waja wazito na wazazi kutumia huduma hizo. Aidha, niliendeleza juhudi za kudhibiti mambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa vijana na kusaidia yatima na watoto wengine waishio katika mazingira magumu.

Jioni ya leo ninayo furaha kuwaelezeni kwamba tumepiga hatua kubwa katika kutimiza dhamira yangu hiyo na malengo tuliyojiwekea.

Elimu:

Tumeendelea na programu yetu ya kutoa ***fursa*** za masomo (scholarship) kwa wastoto wakike hasa wale wanaotoka katika familia maskini na walio yatima. Wanafunzi wa kike 240 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara, na Zanzibar wameweza kunufaika kwa kulipiwa ada na kupatiwa mahitaji mbalimbali ili kuwawezesha kuhudhuria masomo yao ya sekondari (kidato cha I hadi IV). Mwaka jana (2010) kundi la kwanza la wasichana 126 tuliowasaidia walimaliza salama na kufanya mtihani wa kidato cha nne. Tunasubiri majibu yao kwa shauku kubwa. Ni dhamira yetu kuongeza fursa hizo kwa wasichana wengi zaidi kadri rasilimali zinavyopatikana.

Pamoja na mpango huo, nafurahi kuwajulisha kuwa Machi mwaka jana (2010) shule yetu ya Sekondari (WAMA –Shule ya sekondari WAMA Nakayama) ilipokea na kusajili wanafunzi wa kidato cha kwanza. Walio wengi miongoni mwao ni yatima na watoto wengine wanatoka katika mazingira magumu. Wanafunzi hawa wanatoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Kutokana na mazingira yao, taasisi inawapatia mahitaji yao yote ya msingi zikiwemo sare, vitabu, madaftari na nauli. Katika wiki mbili zijazo tunatarajia kupokea watoto wengine 90, watakaoingia kidato cha kwanza. Tunashukuru kwa mandeleo haya, tutaongeza juhudi na tunayo mategemeo zaidi.

Wageni waalikwa,

Uboreshaji Afya

Nikiwa mshirika wa Kampeni ya Wake wa Maraisi wa Afrika Kupambana na UKIMWI (OAFLA), naendelea na kampeni yetu ya kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa vijana. Tumetumia vyombo vya habari kutoa ujumbe muhimu kwa jamii juu ya kurudisha maadili ya kuwakinga watoto wetu kwa pamoja tukitumia kauli mbiu ya ***" Mtoto wa Mwenzio ni mwanao, Mkinge na UKIMWI".***

Mwaka uliopita tulipanua wigo wa shughuli zetu za uraghbishi (advocacy) katika kudhibiti maambukizi ya VVU kwa watoto wanaozaliwa kwa kupitia kampeni maalum ya ***"Save the Unborn Child".*** Katika kutekeleza kampeni hii tumeweza kushirikiana na mradi wa International Centre for AIDS Care and Treatment Program (ICAP) pamoja na Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation (EGPAF) katika kutekeleza miradi ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Aidha nimefanya mikutano ya kuhamasisha jamii katika vijiji mbalimbali nchini kushiriki katika kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi.

Tumetoa vifaa mbalimbali vya huduma ya uzazi katika vituo vya afya 66 vyenye uhaba wa vifaa hivi ili kuboresha huduma hiyo.

Nimeweza kuzunguka mikoa yote ya Tanzania, na kupata fursa ya kuzungumza na wanafunzi, walimu, wazazi na wanajamii juu ya majukumu yao katika kuwalinda wanafunzi wakike dhidi ya mimba za utotoni na vijana kwa ujumla dhidi ya UKIMWI. Halikadhalika tumeshirikiana na shirika la EngenderHealth kutoa mafunzo kwa wanafunzi na walimu katika shule 20 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kuzuiya mimba za utotoni na VVU miongoni mwa wanafunzi.

Uwezeshaji Wanawake

Katika kipindi hiki tumefanikiwa kutoa misaada ya kiuchumi kwa vikundi 88 nchini kwote zikiwemo SACOS na VICOBA. Aidha, tumetoa mafunzo ya uzalishaji na ya ujasiriamali kwa wanawake 1,334.

Ndugu zangu,

Mafanikio haya yanatokana na juhudi na ushirikiano mzuri ninaopata kutoka kwa wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa taasisi ya WAMA.

Aidha, inatokana na ushirikiano na misaada tunayopata kutoka kwa wafadhili wetu mbalimbali ambao napenda kuwashukuru sana.

Ndugu zangu, wageni waalikwa,

Pamoja na mafanikio mazuri tuliyopata napenda kukiri kwamba bado jamii yetu inayo mahitaji mengi ambayo tunapaswa kuyafanyia kazi.

Msaada na ushirikiano wenu ni muhimu ili kwa pamoja tuweze kuishinda vita hii na hatimaye kutoa fursa kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kutumia mapato yao kwa faida yao na familia zao.

Naamini kwa kutumia nafasi zenu, ujuzi na uzoefu kwa pamoja tunaweza kufanya kazi kubwa na ya kujivunia. Kikubwa tunachotakiwa kukizingatia kwa sasa ni kuunganisha ujuzi, rasilimali na uzoefu wetu ili tuweze kuwasaidia wale wenye kuhitaji. Kwa kuwa sote tu wakereketwa wa masuala ya wanawake, ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana katika kuzikabili changamoto zilizopo mbele yetu katika kufanikisha maisha bora kwa wanawake na watoto katika jamii zetu.

Dhamira yetu ni kuendeleza hayo kwa wigo mpana zaidi katika kipindi kijacho kwa mujibu wa malengo yetu ya taasisi.

Wageni waalikwa,

Naomba kwa mara nyingine tena niwashukuru wote kwa dhati kwa michango yenu ya hali na mali kwa WAMA katika kuufanya mwaka wa 2010 kuwa na mafanikio kwetu. Aidha, naomba tuendeleze ushirikiano mwema tuliouanzisha ili tuweze kuleta neema na matumaini zaidi kwa wanawake wanaohitaji msaada wetu.

Nakutakieni heri na Mafanikio katika mwaka wa 2011.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.